

HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA



**Mhe. Mwenyekiti na Wajumbe,
Baraza la Madiwani.**

**TAARIFA YA MKURUGENZI KATIKA MKUTANO WA BARAZA LA
MADIWANI KWA KIPINDI CHA ROBO YA NNE (APRILI - JUNI)
MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KWENYE KIKAO CHA TAREHE
25/08/2022**

1.0. UTANGULIZI

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mujibu wa Kanuni za kudumu za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela za Mwaka 2014, Mkurugenzi anawajibika kulitaarifu Baraza la Madiwani kwa kutoa Taarifa ya Matukio mbalimbali ambayo yamefanyika au yanatarajia kutokea katika kipindi cha kila Robo ya Mwaka. Hivyo, Taarifa hii itagusa Maeneo yafuatayo:-

- i. Taarifa ya Mhe. Mkuu wa Mkoa na Katibu Tawala Mkoa kujitambulisha katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela
- ii. Taarifa ya Zoezi la Sensa ya Watu na Makazi
- iii. Taarifa ya Makusanyo ya Mapato ya Halmashauri kwa Robo ya Nne.

- iv. Taarifa ya Mtihani wa kidato cha sita mwaka 2022
- v. Taarifa ya ugawaji wa madawati
- vi. Taarifa ya upimaji wa Viwanja 3,500 maeneo ya Igalagala, Ilekako, Nyafula, Lugeye na Sangabuye.
- vii. Taarifa ya ufunguzi wa Stendi ya Mabasi na Malori Nyamhongolo.
- viii. Taarifa ya Mapokezi ya Magari.

2.0. TAARIFA ZA MATUKIO MBALIMBALI.

- i. **Mheshimiwa Mwenyekiti**, Mnamo Tarehe 04/08/2022 tulitembelewa na Mkuu wa Mkoa Mpya Mwanza Mhe. Adam Kighoma Ali Malima pamoja na Katibu Tawala Mkoa Ndg. Elikana Mayuganya Balandya katika ziara ya kujitambulisha na kuongea na watumishi wa Halmashauri.
- ii. **Mheshimiwa Mwenyekiti**, kazi ya kuratibu zoezi la Sensa ya Watu na Makazi linaendelea. Zoezi lilianza rasmi siku ya kuamkia Tarehe 23 Agosti 2022 na bado Zoezi linaendelea.
- iii. **Mheshimiwa Mwenyekiti**, Halmahauri kwa Robo ya Nne yaani mwezi Aprili, Mei na Juni iliweza kukusanya jumla ya sh.2,806,480,100.50
- iv. **Mheshimiwa Mwenyekiti**, Mtihani wa kitaifa kidato cha Sita ulifanyika kuanzia Tarehe 9 - 27/05/2022 katika Vituo 8. Jumla ya Wanafunzi 786 Wavulana 213 na Wasichana 573 walifanya mtihan huo.

Daraja	Wavulana	Wasichana
I	29	104
II	84	289
III	86	176
IV	9	4
0	5	0
JUMLA	213	573

- v. **Mheshimiwa Mwenyekiti**, mnamo Tarehe 31/05/2022 Mhe, Mkuu wa Wilaya alitisha hafla ya chakula cha hisani kwa Taasisi, Wafanyabiashara, Watu binafsi na Halmashauri kwa lengo la kukuchangisha jumla ya Madawati 1,526 kwa Shule za Msingi za Wilaya ya Ilemela. Tarehe 26/07/2022 aligawa Madawati 431 katika Shule mbalimbali na jumla Madawati 1,095 yanaendelea kutengenezwa kwa Fundi.
- vi. **Mheshimiwa Mwenyekiti**, Mradi wa kupima, kumilikisha na kupanga Viwanja katika maeneo ya Igalagala, Ilekako, Nyafula, Lugeye na Sangabuye umekamilika. Tulipokea mkopo wa Sh.3,589,774,000/- kutoka Wizara ya Ardhi kwa kazi hiyo. Ulipaji wa fidia na matumizi hadi sasa umefikia Sh.2,232,157,141.40. Bei ya Viwanja hivyo imetangazwa na tunakaribisha Watanzania wote wenye nia ya kununua wanunue sasa Viwanja.
- vii. **Mheshimiwa Mwenyekiti**, Natoa Taarifa katika Baraza lako kuwa Stendi ya Mabasi na Maegesho ya Malori Nyamhongolo imekamilika kwa asilimia 100 na kwamba ilianza kutoa huduma rasmi siku ya Jumanne tarehe 16/08/2022.

- **Mheshimiwa Mwenyekiti**, Halmashauri imepokea Magari 2 aina ya *Land cruiser Hard top* kati ya Magari 4 yaliyonunuliwa na Halmashauri mwaka wa fedha 2021/2022.

heshimiwa Mweyekiti, naomba kuwasilisha.



Eng: Modest J. Apolinary

MKURUGENZI WA MANISPAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA